

HOTUBA YA:
SHEIKH-E-TARIQAT AMEER-E-AHLESUNNAT MUANZILISHI WA
DAWAT-E-ISLAMI HAZRAT ALLAMAH MAULANA ABU BILAL
MUHAMMAD ILYAS ATTAR QADIRI RAZAVI ذامت
برکاتہم
العالیہ

JUMBA LILILO ACHWA

Yaliyomo:-

Kijumba cha mwanzi

Andiko kama onyo

Alilia baada ya kuona jumba la fahari

Kufikiria mauti



Kimechapishwa na : Maktaba-tul-Madina

أَلْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ وَالصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ عَلَى سَيِّدِ الْمُرْسَلِينَ
 أَفَاتَبَعُوا! فَأَعُوذُ بِاللَّهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

JUMBA LILILOACHWA (GOFU)

Mpendwa wa Allah, Bwana Mtume عَزَّوَجَلَّ وَصَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ amesema, “Mwenye kuniswaliya mara elfu moja kwa siku moja hatakufa mpaka aonyeshwe mahali pake Peponi.”. (At'targheeb wat'tarheb, Hadithi ya 2483, J2, Uk. 499 Dar ibn -Katheer).

صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ!

Sayyiduna Junaid Baghdadi عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللَّهِ الْهَادِي anasema 'siku moja nilifanikiwa kwenda mji wa Quufah. Nilipofika niliona jumba kubwa la tajiri moja la kifakhari, milangoni mwake walikuwa na wajakazi wengi. Kwenye uga wa jumba hilo, katika dirisha moja ya nyumba hii, mtumwa mmoja wa kike akiimba nyimbo hii:

**“Ee nyumba. Huzuni
 isikujie, watu waishiyo
 ndani yako wasiangamie!**

أَلَا يَا دَارَ لَا يَدُ خُلَّتْ حُزْنُ

وَلَا يَعْبَثُ بِسَاكِنِكَ الرَّمَانُ

Baada ya mda nilipopita karibu na jumba hilo nikaona milango yake imechafuka, wajakazi hawakuweko na jumba hilo lilionyesha athari ya kuharibika.

Jumba lililokuwa na furaha na shangwe likawa jumba la huzuni na simanzi. Nilipoulizia khabari ya hilo jumba niliambiwa kuwa mwenyewe alifariki na wajakazi wakaondoka. Jumba hilo lilikuwa la upweke na vicheko vya watu vilizimwa na kimya cha kimauti.

Sayyiduna Junaid Baghdadi عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللَّهِ الْهَامِيْ anasema: Nilibisha mlango nikamsikia ajuzua aliekuwemo ndani nikamuuliza “Uzuri wa jumba hili na umaridadi wake umekuwaje? Ufahari wake wote uko wapi? Wakaazi wake wako wapi? Aliposikia hivi ajuzua alianza kulia na akanihadithia yaliyotokea kwenye jumba hilo. Alisema, ‘Wakaazi wa jumba hili waliishi humu kwa muda mfupi. Khatima yao iliwatoa humu na kuwapeleka kwenye makaburi yaliyo na giza. Utajiri na vitu vyote vya mwenye jumba hili vimeanza kuoza. Hii si habari mpya ninayowaelezeni: ni kawaida ya ulimwengu huu. Yeyote anaeishi na akashughulika na anasa mwishowe hufa kwa uchungu na kutupwa kwenye maziara ya upweke. Anategemea, dunia, mwishowe dunia humuacha. Sayyiduna Junaid Baghdadi alisema, Nilipokuwa nikipita karibu na jumba hili hapo mwanzoni mwanamke alikuwa akiimba.

**“Ee nyumba. Huzuni
isikujie, watu waishiyo
ndani yako wasiangamie!**

الْأَيَادِ لَا يَدُ خُلِّقَ حُزْنَ
وَلَا يَعْجَبُ بِسَأَلِكِ الزَّمَانِ

Ajuza akaanza kulia akisema, ‘Mimi ndie yule mwanamke niliyekuwa nikiimba nisiyekuwa na bahati. Mimi niliyebaki kwenye jumba hili la ukiwa. Akatoa sauti kubwa akisema, “Majuto kwa yule aonaye yanayotokea ulimwenguni na bado akaghafilika na kifo chake” (*Rauzur rayyaheen, uk. 110 Dar-ul-Mutba’tul Maymanih Egypt*).

ONYO KWETU SOTE

Enyi ndugu zangu Waislamu! Kisa hiki cha Jumba lililoachwa na wakaazi wake ni funzo kwetu sote! Wakazi hao walipotea katika kuipenda ulimwengu na hawakuogopa mwisho wao. Walijishughulisha kwa kujenga majumba makubwa na kuyapamba. Walishughulikia kung’arisha nyumba zao walisahau makaburi yawangojea. Walizama katika kutafuta marafiki na kazi za wajakazi wao na wakasahau upweke wa kaburi. Mara tu, mwisho wao ukafika na tamaa zao za maisha zikakatizwa. Nyumba zao za furaha na shangwe ziliwachwa tupu na mauti. Walitolewa kwenye nyumba zao zenye taa wakapelekwa kwenye makaburi yenye giza. Jana walikuwa wakistarehe na familia zao na

marafiki, leo wakiwa na huzuni na woga kwenye ukimya wa makaburi yao.

HILA ZA DUNIA

Katika mwisho wa kisa hiki kuna mawaidha mengi ya Madani yanayotuonya lakini ni masikitiko kwa yule anayezijua hila za dunia (za kumpotosha), lakini pamoja na hayo akasahau kufa kwake, kaburi lake na siku ya hukumu na akawa hafanyi mambo yenye kumpendeza Allah عَزَّوَجَلَّ. Mtu huyo anastahili kulaumiwa. Ili tuelekane na hila hii ya duniani, Mola wetu عَزَّوَجَلَّ anatuonya. Amesema Allah عَزَّوَجَلَّ katika Juzuu ya 22, Suratul Faatir, Aya ya 5

Enyi watu ! hakika ahadi ya Mwenyezi Mungu ni kweli. Basi yasikudanganyeni maisha ya dunia, wala mdanganyifu asikudanganyeni juu ya Mwenyezi Mungu.

يَا أَيُّهَا النَّاسُ إِنَّ وَعْدَ اللَّهِ حَقٌّ فَلَا تَغُرَّبَكُمُ
الْحَيَاةُ الدُّنْيَا وَلَا يَغُرَّبَكُمُ بِاللَّهِ الْعُرُوفُ

Bila shaka yeyote anayejua kufa na vituko baada yake hawezi akawa amezama katika uwongo wa huu ulimwengu.

KIBANDA CHA MWANZI

Imehadithiwa kuwa Sayyiduna Nuh عَلَى نَبِيِّنَا وَعَلَيْهِ الصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ alianza kuishi kwenye kibanda kilichojengwa na

mwanzi. Mtu mmoja alimwambia kuwa ingekuwa bora kama ungekuwa na nyumba kubwa. Sayyiduna Nuh عَلَى نَبِيِّنَا وَعَلَيْهِ الصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ alijibu, 'Nyumba hii ndogo inatosha kwa yule mtu ambae atakufa (anaezingatia mauti)! (*Al'aqdul fareed, J3, Uk 146, dar ahyatut turaathul arabi Beirut*).

Inahuzunisha kuwa hatuzingatii mauti lakini tunashughulikia ujenzi wa majengo makubwa. Tunashughulika kujenga vyoo vya kiingereza, majiko ya kimerikani, sakafu za marumaru, makabati makubwa ya kuweka nguo, na mambo mengi ya kisasa. Mshairi wa Arabuni amejaribu kututanabahisha katika mashairi yake yasemayo:

زَيْتٌ بَيْتِكَ جَاهِلًا وَعَمْرُوتَهُ وَلَعَلَّ غَيْرِكَ صَاحِبُ الْبَيْتِ
 مَنْ كَانَتْ الْآيَامُ سَائِرَةً بِهِ فَكَانَتْ قَدْ حَلَّتْ بِالْمَوْتِ
 وَالْمَرْءُ مُرْتَهَنٌ بِسَوْفٍ وَلَيْتَ وَهَلَاكُهُ فِي السَّوْفِ وَاللَّيْتِ
 فَلِلَّهِ دُرٌّ فَتَى تَدَبَّرَ أَمْرَهُ فَعَدَا وَرَاحَ مُبَادِرَ الْمَوْتِ

Tafseer:-

- (1) (Hali ya dunia na fikra za Akherah). Katika mughafalah unashughulika kuipamba na kuishi kwenye nyumba na (ukifariki) labda mtu wa kando ndiye atakayekuwa na nyumba hiyo.
- (2) Kila anaendelea kuishi, ni kama aliyefariki - karibuni atakufa.

- (3) Wanaadamu wamepotea wakiwa na tamaa za mapato ya kilimwengu ijapokuwa tamaa hizo hizo zimeandamwa na mauti.
- (4) Allah ndiye anayejuwa malipo ya yule barobaro aliye na wasiwasi (kuhusu maisha yake ya kaburini na akhera) usiku na mchana na wakati wote hujitayarisha.

Soma habari ifuatayo kutoka kwa Abu Da'wood Shareef ielezayo jinsi Mahbub-e-Rabb-ul-Alameen عَزَّوَجَلَّ وَصَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ alivyokuwa hayapendi majumba makubwa.

JENGO REFU LABOMOLEWA

Sayyiduna Anas رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ anahadithia: Siku moja tulikuwa na Rasoolullah صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ. Bwana Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ akaona jengo refu akauliza, ni nini hii? Mtu mmoja akijibu, hii ni nyumba ya mtu fulani. Aliposikia hivyo Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ hakusema kitu. Mwenye jengo hilo akaja na akatoa salaam kwa Bwana Mtume, Mwenye Taji la Madinah صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ aliyekuwa pamoja na sisi. Nabii صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ akageuza uso wake na hakumjibu salaam yake. Bwana huyu alirudia kutoa salaam mara kadha na akajua kuwa Mfalme wa Madinah Mtume Muhammad صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ

amemkasirikia. Maswahaba عَلَيْهِمُ الرِّضْوَانُ walisema kuwa Nabi صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ alikuwa akitembea na akaliona nyumba lako. Aliposikia maneno haya alienda kulivunja nyumba yake. (*Sunan abu Dawood, Hadithi ya 523, J4, Uk. 402, Dar-ul-Fikr-Beirut*).

Enyi ndugu Waislamu! Hivi ndivyo Maswahaba Kiram عَلَيْهِمُ الرِّضْوَانُ walivyokuwa na mapenzi na Mahbub-e-Rabb-ul-Alameen عَزَّوَجَلَّ وَصَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ. Bwana Mtume, Mwenye Taji la Madinah صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ hakuamrisha jengo livunjwe wala hakusema haliruhusiwi lakini Swahaba عَلَيْهِمُ الرِّضْوَانُ alihisi Nabii wa Rahmah صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ amemkasirikia kwa hilo jengo na jengo hilo lingekuwa kizuizi baina yake na Nabii wa Rehmah, Mwenye Taji la Madinah صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ kwa hivyo akalivunja. Kuvunja jengo hilo si kupoteza rasilimali au fedha lakini ni kwa kumridhisha Mpenzi wao Mtume Muhammad صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ. Ikiwa kwa kulivunja jengo hilo Habib-e-Rabb-ul-Ibaad عَزَّوَجَلَّ وَصَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ atafurahi basi hilo ni jambo bora zaidi. Sayyiduna Ibraheem Khaleel عَلِيٌّ أَلَيْهِ السَّلَامَةُ alikuwa tayari kumchinja mwanawe kwa kutaka radhi za Allah عَزَّوَجَلَّ. (*Sharh Mishkaat, J7, Uk.21, Naeemi kutub khaana Ghujrat*)

Kisa cha Sayyiduna Isma'eel عَلَى نَبِيِّنَا وَعَلَيْهِ الصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ katika Qura'n ni maarufu. Mitihani hii ilikuwa ni kwa watu wa aina yake. Kwa sasa mtu haruhusiwi kuuwa watoto wake kwa ajili ya kuona hivyo kwenye ndoto. Akifanya hivyo ataingia motoni.

ANDIKO LIKIWA KAMA ONYO

Sayyiduna Abu Zakariyya Teemi عَلَيْهِ رَحْمَةُ الْقَوِيِّ amesema, 'Khalifa Suleiman bin Abdul Malik alikuwa kwenye Masjid-e-Haram alipoletewa jiwe lililokuwa na maandishi. Aliagiza aitiwe mtu anayejuwa kusoma maandishi hayo. Baadaye, Hazrat-e-Wahb bin Munabbih رَحْمَةُ اللَّهِ تَعَالَى عَلَيْهِ alikuja na akasoma yale maandishi, likisema:-'Ewe mwanadamu! Kama ungelijuwa mauti yalivyo karibu usingelikuwa na mipango ya muda mrefu ya kilimwengu na usingeshughulika kutafuta utajiri wa dunia. (Kumbuka!) Ukiteleza utafedheheka na kuona haya siku ya Kiyamah. Rafiki zako na jamaa zako hawatakutaka na utaishi na shida na majonzi. Utatenganishwa na wazazi wako na wapenzi wako. Watoto wako na jamaa zako wa karibu hawatakusaidia. Hutaweza kurudi duniani na hutaweza kufanya amali njema tena. Jitayarishe kwa akhera kabla haujakufikia wakati wa majuto'.
(*Dhammul hawa, sura ya 50, uk 498, Dar-ul-Kutubul ilmiyyah Beirut*).

Enyi ndugu Waislamu! Mwenye akili timamu atafakari wakati ambao umeshampita na atubu kikweli makosa aliyoyafanya. Asidhanie bado ana muda mrefu hapa duniani. Aanze kutenda wema aepukane na fitna za kaburi na adhabu ya Akherah. Usiache wema ukatenda maovu kwa ajili ya jamaa zako na marafiki ama kwa ajili ya pesa, kwa sababu haya yote hayatakufaa kaburini, siku ya mwisho na hata hapa duniani. Wema ndio utakaokufaa.

Enyi ndugu Waislamu! Fikra zetu za akhera inawezekana ikiwa kila wakati tunaikumbuka mauti yetu na tutakapovipa mgongo vitu vya ulimwenguni. Utakapofurahishwa na jambo lolote la kilimwengu lete fikra kuwa, karibuni raha hizo utaziwacha.

KULIA BAADA YA KUTAZAMA NYUMBA YA FAHARI

Siku moja, Sayyiduna ibni Mutee' عَلَيْهِ رَحْمَةُ السَّمِيعِ alitazama nyumba yake ya fakhari, akafurahi, baadaye akaanza kulia. Yeye رَحْمَةُ اللَّهِ تَعَالَى عَلَيْهِ akasema, 'Ee nyumba mzuri! Ninaapa kwa jina la Mwenyezi Mungu kama kusengelikuwa na kifo ningekufurahia sana. Kama ingelikuwa sitapelekwa kwenye kaburi nyembamba ningelijishughulisha na

urembo wa dunia hii. Aliposema haya akalia tena. (It'tahaafus saadaatil muttaqeen, j 14 Uk 32 Dar-ul-Kutubul Ilmiya)

MALAIKA WA MAUTI ALISEMA

Imesemekana kuwa malaqal-mauti Izraeel عَلَيْهِ الصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ alikuja kuchukua roho ya mtu. (Mtu huyo) akamuuliza “Wewe ni nani? Malaqal-mauti عَلَيْهِ الصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ akimjibu, ‘Mimi ni yule ambae siwaogopi wafalme, sizuiliwi na mabawabu (walinzi) wa nyumba, na sipokei hongo wala siikubali’. Yule mtu akasema, “Basi wewe bila shaka ni Izraeel عَلَيْهِ الصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ. Hata bado sijajitarisha kwa mauti wala Akherah”. Izraeel عَلَيْهِ الصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ akasema, “Ewe mtu! Jirani yako fulani yuko wapi? Rafiki yako fulani yuko wapi? “Walifariki”. Izraeel عَلَيْهِ الصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ akasema, ‘Hukupata funzo lolote katika vifo vyao na ukajitarisha na kifo chako? Baadaye akatolewa roho. (Almustatrif, J2, Uk 474, Dar-ul-Fikr Beirut)

Enyi ndugu Waislamu! Waliofaulu na wenye akili ni wale wanaposhuhudia mauti ya watu wengine hufikiria mauti yao na kisha huanza kujitarisha na kaburi, na Akherah. Mababu zetu wachamungu رَحْمَةُ اللَّهِ تَعَالَى walikuwa wakisema, ‘Amebahatika anaejifunza kwa wengine”. (It'tahaafus saadaatil muttaqeen, J14, Uk. 32, Dar-ul-Kutubul Ilmiya Beirut).

KUFIKIRIA MAUTI

Kufikiria mauti kimzaha haitakusaidia kwa vile siku zote twaona watu wakifa na hata tunashuka makaburini kuwazika. Njia bora ya kufikiria mauti ni mtu akae peke yake na akasahau mambo ya kidunia. Jaribu kukumbuka sura za marafiki, ndugu na jamaa ambao wameshafariki. Wakati huo huo zingatia shughuli walizokuwa nazo ulimwenguni, namna walivyokuwa na bidii ya kutafuta maisha mazuri, elimu ya juu na ndoto zao za baadaye za maisha yao.

Pamoja na shida zote za kiulimwengu walijikusudia kudumisha kazi zao. Walipenda raha za dunia na walifurahia mapumziko yao. Waliishi kama kwamba hawataondoka na wakajisahau katika anasa za dunia. Katika kughafilika kwao mara ikawakumba kifo na kupelekwa makaburini. Wazazi wao walijawa na huzuni, wajane wao hawakuwa na watu wa kuwaangalia, watoto wao walibaki wakilia, ndoto zao zilikatizwa, mipango yao ilivunjika na kazi zao za duniani hazikumalizika. Shughuli zao za kilimwengu zimekuwa vumbi tupu. Warithi wao wamewasahau. Baada ya kufikiria haya zingatia hali yao ilivyo kaburini na kwamba mifupa yao tu ndio iliyosalia. Namna gani nyuso zao zilivyofujika.

Walipokuwa wakitabasamu ilikuwa ni kama ua linalochomoza, lakini kwa sasa meno yao yameoza na kung'oka, midomo yao imejaa usaha, macho yao mazuri makubwa yamepasuka na kutiririka kwenye mashavu yao. Nywele zao za ondo (laini) zimeng'oka. Mabuu yatambaa kwenye pua zao dhaifu. Midomo yao kama waridi sasa imeliwa na minyoo. Watoto wadogo wasio na makosa wenye maneno matamu ndimi zao zimejaa wadudu. Nguvu na mwili mzuri wa barobaro utakuwa si chochote. Viungo vitakuwa mbali mbali.

Baada ya kuyatafakari haya yote uyakinishe kuwa hali yako itakuwa kama hivyo karibuni. Hivi karibuni nitayapata machungu ya mauti, macho yangu yataangalia juu na wapenzi wangu wote watakuwa karibu yangu,

'Mpendwa wangu, mpendwa wangu'. Baba atapiga kelele, 'Mwanangu mwanangu' dada zangu watasikika wakipiga mayowe, "Kakangu kakangu'. Wapendwa wangu watalia kwa kite. Katika kelele hizi roho yangu itakuwa ikitolewa. Mtu mmoja atayafunga macho yangu anifinike mwili wangu kwa nguo. Mwoshaji ataitwa, ataniweka ubaoni (au kitandani) ili kuniosha na baadaye kunivisha sanda. Huku watu wakilia jeneza langu litatolewa nyumbani nilimokuwa nikiishi. Waliokuwa

wakijigamba kwa ajili yangu watanisindikiza kaburini. Nitawekwa kaburini na wapendwa wangu wanifukie kwa mchanga. Wataniacha peke yangu na hakuna mtu atakayebaki kando ya kaburi langu kuniwaza. Mwili wangu utanza kuoza humo kaburini. Minyoo wataanza kula sikio la kiume au la kushoto? Wataanza kula ulimi wangu au mdomo wangu? Minyoo itasambaa inapotaka. Wataingia puani, machoni, na masikioni mwangu. Fikiria yote haya na kuja kwa malaika, maswali yao na adhabu za kaburini. Ukifikiria kufa kwa namna hii (**Fikr-e-Madina**), In'shaa-Allah عَزَّوَجَلَّ utanza kujiandaa na mauti. Utataka kufanya mema kwa wingi na utajiepusha na madhambi. Kuikumbuka mauti, sikiliza kaseti ya "Jumba lililoachwa (Viran Mahal)' hata kama ni mara moja kila mwezi na uwe pekee yako umekaa kwenye giza. Inshaa-Allah عَزَّوَجَلَّ itakusaidia sana. Enyi ndugu Waislamu! Mababu zetu waliokuwa wachamungu رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى daima walikuwa wakifikiria mauti, kaburi na siku ya mwisho. Ni kwa ajili hii waliweza kuepuka na dhambi na daima walikuwa wakifanya wema. Badala ya kushughulika zaidi na ulimwengu, walikuwa wakilia kwa kumcha Allah عَزَّوَجَلَّ.

صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ!

USIKU WA KWANZA KWENYE KABURI

Sayyiduna Yazeed Raqashi عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللَّهِ الشَّافِعِيّ amesema “tulilmwendea Amir Bin Abdullah عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللَّهِ تَعَالَى alikuwa akilia sana na tukamuuliza sababu ya kilio hicho. Yeye عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللَّهِ تَعَالَى akajibu, ‘Nachelea usiku huo ambao mapambazuko yake ni siku ya hukumu’, inaonyesha kuwa usiku wa kwanza kaburini ni jambo lenye kuniogopesha (*Almajaalasa, J1, Uk 199, Dar-ul-Kutubul Ilmiyyah Beirut*).

Enyi ndugu Waislamu! Wakizingatia siku ya hukumu, Wachamungu wetu عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللَّهِ تَعَالَى wanatutanabahisha tujiandae na kifo.

KWA NINI KUFIKIRIA MAUTI NI MUHIMU!

Hujja-tul-Islam Sayyiduna Imam Muhammad Ghazali عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللَّهِ الْوَالِيّ ameandika katika Ihya-ul-Uloom, ‘Mtu mwenye kuamini kuwa kifo ni lazima, anaeamini kuwa mchanga ndio tandiko lake, kwamba kaburi ndio marejeo yake, kwamba wadudu ndio watakaokuwa rafiki zake, kwamba siku ya hukumu itakuwa shahidi kwake na pepo au moto ndio marejeo yake ya mwisho, basi na azingatie na kufikiria mauti mara kwa mara na kujiandaa. Kuna msemu usemao, ‘Lolote lisilo na

budi kuja liko karibu.’ (*Ihya-ul-Uloom, J4, Uk. 475, Dar-ul-Kutubul Ilmiyyah Beirut*).

Bwana Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ amesema, ‘Mwenye akili ni yule anayejihisabia matendo yake na akajiandaa na mauti na yale ya baada ya umauti’ . (*Jamiu’ Tirmizi, Hadith ya 2467, J4, Uk. 207, Dar-ul-Fikr-Beirut*).

Wachamungu رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى walikumbuka umauti mara nyingi na wakati mwengine walizimia wakifikiria umauti na siku ya Hisabu.

JAWABU KUHUSU HALI YA AFYA

Mtu alipokuwa akimuuliza Sayyiduna Yazeed Raqaash رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ kuhusu hali yake, yeye رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ alikuwa akijibu, ‘mtu atakuaje ambaye kifo chake kimepangwa wakati maalum; ambaye marejeo yake ni mchangani, kaburi litakuwa nyumba yake, wadudu wawe rafiki zake pamoja na hayo, vitisho vya siku ya kiyama anayoingojea hali yake itakuwaje? Baada ya kusema maneno haya alikuwa akianza kutetemeka na kulia zaidi mpaka kupoteza fahamu. (*Almustarif, J2, Uk 477, Dar-ul-Fikr Beirut*).

KUPAMBAZUKA KATIKA HALI GANI?

Vivyo hivyo, mtu mmoja alimuuliza Sayyiduna Malik bin Dinar رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ alivyoamka. Yeye رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ alijibu, ‘Wewe unaniuliza asubuhi yangu

itakuwaje alfajiri ya yule aliyekaribu kugura nyumba hii (yaani-dunia) hadi nyengine (yaani Akherah) akiwa hajui maskani yake ni pepo au moto'. (*Tanbi-hul-ghafileen, Uk 56, Dar ibn -e-Katheer Beirut*).

Wapenzi waislamu! Tuwe na fikra za watu wema na tufuate mfano wa watu hawa waliokuwa wema رَحْمَهُمُ اللَّهُ تَعَالَى na tujitayarisha kwa umauti badala ya kushughulika zaidi na ulimwengu ulio na mwisho.

ZAWADI BORA

Katika khutba moja, Sayyiduna Umar ibin Abdul Aziz عَلَيْهِ رَحْمَةُ الْعَزِيزِ alisema, 'Enyi watu! Dunia hii si nyumba yenu ya milele. Allah عَزَّوَجَلَّ ameshatoa hukumu kuwa dunia hii itamalizika na watu wake watagurishwa. Kwa kipindi kifupi kinachokuja, majumba haya makubwa yataharibiwa na kuachwa. Kila mtu ataondoka. Enyi watu, Allah عَزَّوَجَلَّ awahurumie, mkiondoka ulimwenguni, ondokeni na zawadi mzuri (matendo mazuri) katika safari yenu. Zawadi bora ni uchamungu عَزَّوَجَلَّ na kujiepusha na mabaya. (*Ihya-ul-Uloom, J4, Uk 484, Dar-ul-Kutubul Ilmiya Beirut*).

DUNIA ITAHARIBIWA!

Wakati mmoja katika khutba yake, Sayyiduna Imam Shafii رَحْمَةُ اللَّهِ تَعَالَى عَلَيْهِ alisema, "Kwa hakika dunia

ni mahali panapofanyiwa makosa na ni nyumba ya aibu na fedheha. Wakaazi wake watafishwa na kupelekwa makaburini, mapitio ndio tija yake, na utajiri wake karibuni utakuwa umaskini wake. Wingi huwa uchache na uchache si lolote. Ogopa ukumbi wa Allah عَزَّوَجَلَّ na tubia na utosheke na ambacho Allah عَزَّوَجَلَّ amekupa. Fikiria malipo ya Akherah badala ya utajiri wa duniani. Maisha yako ni mfano wa kivuli chenye kupita na ukuta unaoanguka. Zidisha amali zako za dunia hii.' (*Al-Zuhad wa qasrul amal, uk 61, Maktaba-ul-Ghazali Damascus*)

LEO NI SIKU YA VITENDO!

Alipokuwa akitoa khutba huko Quufah, Sayyiduna Ali ul- Murtadha كَرَّمَ اللهُ تَعَالَى وَجْهَهُ الْكَرِيمِ alisema, 'Mimi nahofia kuwa mtaanza kuwa na matamanio. Tahadharini! Mkifuata matamanio yenu kutakutoweni kwenye njia ya haki. Karibuni dunia itawaacha na akhera itawafikia. Maisha haya (ya duniani) ni maisha ya vitendo, sio ya Hisabu, na maisha ya kesho (Akherah) ni maisha ya hisabu, sio ya vitendo! (*Al-Zuhad wa qasrul amal, uk 58, Maktaba-ul-Ghazali Damascus*)

DUNIA NI MAANDALIZI YA AKHERA

Hazarat Sayyiduna Uthman -e- Ghani رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ katika khutba yake ya mwisho anatusihi yakuwa:

'Allah عَزَّوَجَلَّ ametuleta hapa duniani ili tujiandae kwa ajili ya Akherah na si kupotea katika anasa za dunia. Bila shaka dunia itafika mwisho wake na Akherah itadumu maisha milele.

Ulimwengu huu unaopita isiwapanye kughafilika na Akherah itakayodumu milele. Usiupe kipao mbele ulimwengu huu wenye kumalizika, kuliko Akherah itakayokuweko milele, kwa sababu dunia hii karibuni itamalizika na Akherah ndiyo itakakayo baki milele na mutarudi kwa Allah عَزَّوَجَلَّ.

Basi Mcheni Allah عَزَّوَجَلَّ muepukane na adhabu na muwe karibu naye.

MARAFIKI WEMA KIFO KIZURI

Tikiti huliangalia tikiti jingine na likapata rangi yake. Tembe ya ufuta ikitumbukizwa ndani ya waridi huwa na uwezo wa kupata tabia za waridi. Hali kadhalika mtu mwenye roho ngumu kama jiwe hupata tunu ya kuwa kama almasi pindi anapo dumu kubakia ndani ya jumuiko la Dawat-e-Islami hivyo basi akawa anajaa mapenzi ya Allah عَزَّوَجَلَّ na Mfalme wa Madina صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ. Wengine hata huaga dunia huku wakitabasamu na watu wa kawaida wakatamani ingelikuwa wao.

Inaelezwa kwamba katika Tandu Allah Yaar (Sindh) mtu mmoja alijiunga na Dawat-e-Islami na akawa na tabia ya kuswali Swala zake tano pamoja na jamaa ya Aashiqane-Rasool (wapenzi wa mtume). Vile vile alijiandikisha jina lake miongoni mwa wale walio kaa siku kumi I'tikaf, miongoni mwa wale ambao ndevu zao hazitokatwa chini kiasi cha kiganja cha mkono, miongoni mwa wale watakao vaa kilemba cha kijani, miongoni mwa wale watakao jiunga na ijtimai ya kila wiki na kuahidi kusafiri na Dawat-e-Islami ndani ya Madani Qafilah. Kwa ufupi akapata mabadiliko ya Madani ndani yake, akanyenyekea kwa Allah عَزَّوَجَلَّ kwa kutaka maghfira kutokana na dhambi zake zilizo pita na kujibidiisha kuishi kulingana na Sunnah za Mfalme Wa Madinah صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ.

Siku moja kwa bahati mbaya alichomeka vibaya sana kiasi kwamba kulingana na ripoti ya watabibu asilimia themanini (80%) ya mwili wake ulikuwa umeteketea. Jambo la kushangaza ni kwamba wageni walio mtembelea badala ya kutarajia malalamiko kutoka kwake waliona mgonjwa huyu amezama katika Dhikr na Durood (Kumswalia Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ). Pia alikuwa anaomba Dua na kusoma Surah za Qur'an alizozihifadhi kwa moyo, pindi alipokuwa amejumuika pamoja na kundi la

Dawat-e-Islami. Aliendelea hivi hivi kwa kipindi cha masaa 48 na kulipo adhiniwa kwa Swala ya Al-Fajr alipokuwa akisoma. لا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ مُحَمَّدٌ رَّسُولُ اللَّهِ akaaga dunia. Allah عَزَّوَجَلَّ amrehemu na atughufirie kwa ajili yake.

IJTIMA'A

Hudhuria Kongamano La Kila Wiki (Ijtima'a) La Dawat-E-Islami Bila Ya Kuchelewa Katika Mji Wenu Kila **Alhamisi** Baada Ya Swala Ya **Maghrib** Katika **Madani Markaz** (Masjid Kanz-Ul-Iman) **Dawat-E-Islami**. Area Tononoka Mvita.

MAKTABA-TUL-MADINA

P. O. Box 287 – 80100, Mombasa-Kenya

Tel : +254 721 521916 / + 254 723 745751

Next To Madani Markaz, Kanzul Iman - Behind KCB Bank-Mvita,
Jomo Kenyatta Avenue, Mombasa

BAADA YA KUSOMA KITABU HIKI MPE MWENZAKO

Eneza vitabu vinavyo chapishwa na Maktaba-tul-Madina kwenye sherehe za ndoa, wakati wa misiba, wakati wa Ijtimai na hata nyakati zingine na ukipatie thawabu ifanye ni ada kuweka vitabu hivi kwenye duka lako kwa min-ajil ya kugawanya bila kulipisha kwa wateja wako wape wauzaji magazeti vitabu hivi, au wape watoto wavieneze kwa majirani zako peana kitabu kila wakati na upate fadhila za kuamrisha mema.

Ikiwa na asilia

kitabu cha 03

JUMBA LILILO ACHWA

ویران محل

Yaliyomo:-

- **Kijumba cha mwanzi**
- **Andiko kama onyo**
- **Alilia baada ya kuona jumba la fahari**
- **Kufikiria mauti**

**Imetolewa na: Majlis-e-Tarajim
(Dawat-e-Islami)**

أَحْمَدُ مُحَمَّدُ رَبِّ الْعَالَمِينَ وَالصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ عَلَى سَيِّدِ الْمُرْسَلِينَ آمِينَ اللَّهُمَّ أَنْعِمْنَا وَأَنْعِمْنَا عَلَى الْوَالِدَيْنِ الْكَرِيمَيْنِ بِشِيرِ الْإِسْلَامِ الْوَالِدَيْنِ الْكَرِيمَيْنِ

Baraka Za Sunnah

سُبْحَانَكَ يَا رَبِّ رَبِّ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ يَا رَبِّ الْعَرْشِ الْعَظِيمِ
Alhamdu Lillah غزوة Sunnah za Bwana Mtume يتسمم
zinafunzwa na kusomwa katika mazingira ya Madani ya
Dawat-e-Islami, shirika la harakati za Qur'an na Sunnah la
kimataifa lisilo jhusisha na siasa. Ijtimai ya kila wiki ya Karachi
(Pakistan) huweko kila Alhamisi baada ya Swalatul-Maghrib
huko Faizan-e-Madina, Mahalla Sodagaran, Old Sabzi Mandi.
Madani inakuomba ushiriki katika Ijtimai hii na ukeshe kwenye
Faizan-e-Madina.

سُبْحَانَكَ يَا رَبِّ رَبِّ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ يَا رَبِّ الْعَرْشِ الْعَظِيمِ
Jitahidi utoke na kundi la Wapenzi wa Bwana Mtume يتسمم
katika Madani Qafila na huku ukileta Fikr-e-Madina, ujaze
kadi yako ya Madani In'aamaat kila siku na umpe zimmadaar
(mwakilishi) wa eneo lako mnamo siku kumi za mwanzo za
mwezi wa kiislamu. In'shaa-Allah غزوة kwa baraka ya kufuata
utaratibu huu, tutaanza kushikamana na Sunnah za Mtume,
Tutachukia maasi na tutailinda Imaani yetu. Kila ndugu muisl-
amu aweke niya kuwa nitajanibu kurekebisha nafsi yangu na
ya watu wa dunia nzima In'sha-Allah غزوة.

Kurekebisha nafsi zetu tutajaza Madani In'aamaat, na ku-
rekebisha watu wa dunia nzima tutasafiri na Madani Qafila-
In'sha-Allah

مكتبة المدينة

MAKTABA-TUL-MADINAH

Faizan-e-Madinah, Mahallah Saudagran,
Old Sbazi Mandi, Karachi, Pakistan. Phc +92(21) 4921389-93-4126999
Email: maktaba@dawateislami.net Web: www.dawateislami.net